BIBLIA KWA TASWIRA, AGANO LA KALE, KITABU CHA 18
WAAMUZI

UASI

(VISUALIZED BIBLE, Vol 18, OT, Rebellion**)**
Mwandishi: Arlene S. Piepgrass
Muchapaji: Vernon Henkel
Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

© Bible Visuals International
PO Box 153, Akron, PA 17501-0153
Simu: 717-859-1131
www.biblevisuals.org

SOMO 1 - UASI WA TAIFA LA MUNGU

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Waamuzi 1:1-5,31; Kumbukumbu la Torati 28:1-68; Zaburi 106:34-48

Shabaa ya somo: Ni kuonyesha kama kuenda mbali na Mungu kunaleta ukosefu na uchafu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Kama Bwana anasikia na kujibu wale wanaotubu kwa kweli na kumurudilia.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kutii Mungu na Neno lake.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kubadirisha tabia zao na hali zao zinazokuwa kinyume na sheria za Mungu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Kiingilio (Torati 7:1-6; 28:1-68; Waamuzi 2:11-16; 3:5-7; Zaburi 106:34-48)
2. Adabu kwa Waisraeli wanaoasi (Waamuzi 4:1-2; 5:6-8)
3. Waisraeli wanatubu na kumurudilia Mungu (Waamuzi 4:3-5)
4. Mungu anahurumia Waisraeli (Waamuzi 4:6-24; 5:20-22)
5. Waisraeli wanasifu Mungu (Waamuzi 5:1-35)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya Mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti" (Mezali 14:12).

Maelezo kwa mwalimu:
Waamuzi – kitabu cha huzuni katika Biblia – kinaeleza muda wa giza katika historia ya Waisraeli. "Waliacha (walienda mbali) Mwenyezi Mungu wa baba zao … na wakatumikia Bali na Astorati (Waamuzi 2:12-13).

Taifa la Israeli walikumbuka:
1. Ukombozi wa Mungu wa kimujiza toka utumwa wa Misri (katika kutoka).
2. Ulinzi na uongozi wa Mungu katika jangwa (Inafafanuliwa katika kitabu cha Hesabu); na
3. Uwezo wake wa kuwapa inchi aliyowaahidi (inaelezwa katika kitabu cha Yoshua)

Mbele Musa akufe, Mungu aliahidi kubariki taifa lake kama wakitii sheria zake (Torati 28:1-14). Aliwapasha habari vilevile ya azabu ya kutokutii (Torati 28:15).

Chini ya uongozi wa Yoshua, Waisraeli waligeuka washindaji na walishinda mataifa yote ya wapagani katika Kanana (Waamuzi 2:7). Kisha kifo cha Yoshua, kizazi kipya wakaasi Bwana (Waamuzi 2:10-13). Waliishi kama watu waovu pa Kanana, walioa Wakanana na pia waliabudu miungu yao.

Kwa kuwaazibu Mungu aliruhusu mataifa adui kushinda taifa la Israeli. Wakati Waisraeli walihuzunika kabisa juu ya zambi zao, walitubu na kuomba Bwana awasamehe. Sasa Mungu aliamusha waongozi wanaoitwa "Waamuzi" kusudi wawasaidie kwa wale waliojiongeza.

Ile iligeuka desturi iliyorudia mara saba katika miaka 330 (Waamuzi 2:11-19; 3:5-11; 3: 12-15; 4:1; 6:1; 10:6; 13:1).

Waisraeli
1. Walienda mbali na Mungu (uasi)
2. Waliadibishwa na Mungu
3. Kutubu – kuomba musamaha kwa Mungu
4. Kusamehewa na Mungu na salama na Mungu

Uendelee kujikumbusha na mufano unakuwa ndani ya jalada ya mwisho. Kama ikiwezekana, weka maneno yanayostahili kwa kila tarakimu.

Mara pili katika kitabu cha Waamuzi, tunasoma, "Kila mtu alifanya maneno aliyoona ni mema mbele ya macho yake" (Waamuzi 17:6; 21:25). Kwa maneno mengine, taifa la Israeli ambalo Mungu alichagua kwa upendo kwa ajili yake mwenyewe, liliasi Mungu. Sawa vile baba anayewapenda, Bwana alipashwa kuadibisha wana wake.

Mafundisho yanayokuwa katika kitabu cha Waamuzi, yanakuwa kwetu leo vilevile. Sisi vievile, tunapashwa kuchagua kutii Mungu kama tukitaka kupata baraka zake. Wakati waamini wanasahau Bwana, wanakataa kutii Neno lake, wanakataa kuishi maisha ya utakaso, wanakuwa waasi mbele ya Mungu. Kwa hiyo kwa kila zambi, Mungu Baba anaazibu waliyo wake (wana wake) (Waebrania 12:5-15).

Kwa wakati wa Waamuzi, tunajifunza juu ya rehema, upendo, uvumilivu na Neema ya Mungu. Wakati tunaenda mbali naye, anachunga kusikiliza maombi yetu ya musamaha na anatupa mwendo mupya (Ona Zaburi 106:44-45; 1 Yoane 1:9).

1. Ingilio (Torati 7:1-6; 28:1-68; Waamuzi 2:11-13; 3:5-7; Zaburi 106:34-48)

<u>Onyesha taswira kwa ngambo ingine ya jalada:</u> Mbele Waisraeli waingiye Kanana inchi ambayo Mwenyezi Mungu aliwaahidi, aliwapatia sheria kamili kwa mukono wa Musa. (Kazia sana ahadi za Mungu na maonyo ya Mungu, Torati 11:26-28; 16:1 hadi 30:20).

Juu ya taswira, andika maneno haya ya lazima: KUTEKA INCHI, KUTUKUZA MUNGU, KUANGUSHA SANAMU. Uhakikishe kama wanafunzi wako walisikia kama Waisraeli walijua mafundisho ya Mungu.

"Musifanye mapatano na taifa mbaya la Kanana" asema Bwana. "Mujitenge nao. MUKAMATE inchi zima. MUTUKUZE tu Mungu anayeishi mbinguni. MUANGUSHE sanamu zao. Musiache wana wenu ao binti zenu kuoa ao kuolewa na wakanana. Wakifanya vile, wana wenu wataenda mbali nami na watatumikia miungu ya Kanana."

Waisraeli Walikuwa taifa maalumu la Mwenyezi. Mupango wake, ulikuwa waishi na kutawala inchi ya Kanana na wawe wengi katika dunia. Alitaka mataifa mengine waone taifa la Israeli sawa mifano ya wale wanaotukuza Mungu wa kweli na aliye hai.

"Kama mukinitii," aliahidi Bwana, "Nitafanya kila kitu kuwa baraka kwenu. Shamba zenu zitatoa matunda mazuri. Nyama zenu zitazidishwa. Mutakua na wana wengi. Jamaa zenu zitakuwa na afya njema."

Mungu anaonya, "Kama mukikataa kunitii, vidudu vitakula mimea yenu. Magonjwa ya kuua yatawazuru. Adui zenu watawashinda na watawatawala na kuwa bwana zenu."

Kama ungelikuwa muIsraeli, ungelichagua kufanya nini? (Tia wanafunzi moyo kuhojeana. Uliza maana ya kuchagua kwao. Onyesha kama kutii Bwana inamaanisha kuwa tofauti, ingawa hakuna mutu anapenda awe tofauti. Uliza ulizo hili, "Utakuwa tayari kutii Neno la Mungu hata kama unazoea wale wasiolipenda?"Taja matendo kamili yanayofanywa na wanafunzi wako. Wizi, uongo, kujivuna, kutumia dawa za kulevya, kutokuenda kanisani, uchawi, kuzola wasioamini, Vh. Uwasaidie kuelewa uchaguzi ambao Waisraeli walipashwa kufanya).

Wakati taifa la Israeli liliingia mara ya kwanza katika inchi ya Kanana, chini ya uongozi wa Yoshua, walitii sheria za Mungu. Bwana aliwapatia ushindi mukubwa. Ukapata sehemu kubwa ya udongo kwa wakati ule.

Lakini, kuliko kuendelea kupiganisha wakanana taifa la Israeli waliunga urafiki na wao na hata walifanya mapatano. Taifa la Israeli likaambia Wakanana, "Inchi hii ni yetu sasa. Lakini munaweza kuishi ndani kama munatutumikia!"

Nini iliyokuwa mubaya katika maneno haya? (Hawakutii Bwana. Aliwaagiza kujitenga na Wakanana wa inchi. Kutokutii ni kuasi. Bado kidogo Waisraeli wataruhusu wana wao kuoa Wakanana. Waliabudu hata miungu ya Wakanana, sanamu za mawe na miti!

Waisraeli walienda mbali na Mungu. Walikuwa waasi.

2. Azabu kwa Waisraeli waasi (Waamuzi 4:1-2; 5:6-8)

Wakati taifa la Israeli lilikataa kutii Bwana na kuenda mbali naye kwa njia ya uasi, Mungu aliinua mufalme Yabini (liwali wa Wakanana) na jemadari wake Sisera kupiga Waisraeli. Watu wale hawakuamini Mungu wa kweli aliye hai. Waliabudu Bali, mungu wao aliyetengenezwa na mutu.

(**Mwalimu:** Kumbusha wanafunzi ubatili wa sanamu zilizotengenezwa na mikono ya watu, Zaburi 135:15-18).

Kwa muda wa miaka 20, mufalme Yabini mukanana, alitawala juu ya taifa la Israeli. Kwa sababu alikuwa mubaya, maisha yao ilikuwa mubaya. Waisraeli waliasi Mungu na waliteswa sababu ya ile.

Watu katika Israeli walikuwa na woga. Na wakati walisema pamoja polepole ndani ya nyumba, hiyo ilikuwa kitu kinachofanana na hiki …

Wanawake walinungunika, "Tuna wog wa kwenda vijijini kwa kutafuta maji sababu waaskari wa Kanana watatuchokoza.

Onyesha taswira 1: Vijana wanaume walisema, "si utaratibu kwetu kusafiri hapa katika Kanana. Wizi wanajificha mahali pote kwa kutushambulia. Tunapashwa kutumia njia zisizojulikana na kuwa wenye kusikiliza na kuchunguza adui zetu."

Wengine walilalamika, "Mufalme Yabini anatulipisha kodi nyingi inayotuma hatueneze mahitaji yetu yote."

Wengi walijiuliza, "sababu gani waaskari wetu hawapiganishe jemadari Sisera na jeshi lake na kutuokoa na Wakanana?"

Waaskari walishangaa. "Munajua namna gani jeshi lake lina nguvu? Anakua na waaskari 300.000 (Kufuatana mwanahistoria Joseph). Anakua na gari za chuma 900! Hatuna hata moja! Tunapigana kwa miguu! Hatuna bahati ya kushinda Sisera. Gari zake zinakatakata watu na vitu!"

"Tufanye nini?" taifa lililalamika. "Nani anaweza kutusaidia?"

3. Waisraeli wanatubu na kurudilia Mungu (Waamuzi 4:3-5)

Nani angeliweza kuwasaidia? (Mungu wa kweli na aliye hai). Lakini mbele Mungu hayawasaidia. Walipashwa kuacha kuabudu miungu ya Wakanana na kuomba Bwana kuwasamehe (Torati 4:29-31)

Onyesha taswira 2: Kwa mwisho, waliomba, "Ee Bwana, tulifanya zambi mbele yako. Tulifanya yote uliyotukataza kufanya. Ikikupendeza utasemehe. Adui zetu ni wenye nguvu. Hatuwezi kuwapiganisha. Ikikupendeza utusaidie!" (Tuone Waamuzi 4:3)

Munafikiri kama Mungu alisikia na kujibu ombi la namna hii? Sikia Neno lake (Zaburi 4:3b; 6:9; 17:6; 18:3; 28:6; 30:1-2; 34:4; 40:17; 50:15; 56:9; 66:18; 106:44; Mezali 28:13. Chagua moja ya aya hizi na uzisome polepole na mbalimbali. Ukazie kama haua ni kwetu sisi vilevile.

4. Mungu anasamehe Waisraeli (Waamuzi 4:6-24; 5:20-22)

Huko kulikuwa mwanamuke mzuri (nabii muke) katika Israeli aliyeitwa Debora aliyependa Bwana na alimutii. Mungu alimuchagua sawa muamuzi (mwongozi) wa taifa lake. Wakati Bwana alisikia taifa lake linaomba musamaha. Akasema kwa Debora yale alipashwa kufanya. Polepole alitii.

Kwanza Debora akaita Baraka kwa kuongoza jeshi "Chagua waaskari 10.000 na mutembee ngambo ya mulima Tabora kwa kupiganisha jeshi la Kanana" aliwaamuru. "Mwenyezi Mungu atavuta Sisera, mukubwa wa jeshi la Yabini, watu wake na gari zake katika muto Kisoni na kuwatia mikononi mwenu."

Baraka akawaza mara moja, kukamata tu waaskari 10.000? Jemadari Sisera anakuwa na waaskari 300.000! Anakuwa na gari 900 za chuma! Wakanana watatuharibu! Debora hawezi kujua mambo anayoyasema.

Lakini Debora aliendelea, "Mwenyezi Mungu atatupa ushindi Baraka! Usiogope"

Lakini Baraka alikuwa na woga. Hauamini Mungu kama Debora. "Nitaenda, kama ukienda na mimi Debora."

"Vizuri sana. Nitaenda pamoja nawe Baraka. Lakini sababu haukuamini Mungu kabisa hautapata sifa ya ushindi. Bwana ataweka jemadari Sisera katika mikono ya mwanamuke."

Wakiongozwa na Baraka pamoja na Debora karibu yake waaskari wa israeli walipanda Mulima Tabora.

Jemadari Sisera, alipopata habari ya mwendo wao, alishangaa, "Namna gani hawa Waisraeli wanapima kuwaza kama wanaweza kuasi mufalme Yabini? Tutaonyesha watumwa kama hawawezi kupingana na sisi!"

Jemadari Sisera aliamuru jeshi lake kujitayarisha kwa vita. Alifanya sawasawa na jinsi Mungu aliambia Debora atafanya. Aliongoza watu wake na gari zake za chuma 900 chini ya mulima Tabori kando wa muto Kisoni!

Kwa wakati ule, Debora aliamuru Baraka, "Amini Mungu. Anatembea mbele yako. Atashinda Sisera – leo, atatuokoa na Wakanana! Shambulia!"

Baraka alishambulia toka juu ya mulima hadi chini akifuatwa na waaskari wake 10.000.

Onyesha taswira 3: Mara moja mvua ikaanza kunyesha, maji ikajaza muto Kisoni. Farasi za Wakanana zikaogopa, zikatupa wale waliozipandia na kuwakanyaga hadi kufa.

Baraka na watu wake walikimbiza Wakanana, wakawaua kwa panga zao. Hakuwa mutu aliyeponyoka ila jemadari Sisera. Alirukia juu ya gari la chuma na kuponyesha maisha yake. Baraka aliwafuatilia na nguvu sana.

Alipokuwa akikimbia, Baraka aliona hema la Heberi na muke wake Yaeli. Heberi alikuwa rafiki wa mufalme Yabini, alifikiri Sisera, kama nikifika pale nitaokolewa!

Yaeli akaita, "Jemadari Sisera, kuja ujifiche ndani ya hema letu." Alikubali kwa furaha mwito wake na alikunywa maziwa ambayo Yaeli alimupa. Akichoka, alishikwa na usingizi mzito.

Yaeli hakuchunga muda murefu. Alikamata musumari wa hema na nyundo mkononi mwake, akapiga musumari kwa paji la uso wa Sisera, akamuua!

Kisha muda mudogo, Baraka akakuja akitafuta jemadari Sisera. Yaeli akaita, "Baraka, hapa kuna mutu anayekutafuta."

Utafikiri nini kama ukichunguza moyo wa Baraka alipotazama jemadari anakufa akipigwa musumari ndani ya hema. (Tazama Waamuzi 4:8-9). Masemi ya Debora ikageuka kweli!

Nani alikuwa chanzo ya ushindi wa Israeli siku ile? Debora, Baraka, Yaeli? (Acha wanafunzi wahojeane. Soma Waamuzi 4:23. Mungu muweza yote alikuwa mushindaji).

5. Waisraeli wanasifu Mungu (Waamuzi 5:1-31)

Onyesha taswira 4: Debora na Baraka walingoza Waisraeli katika kusifu Mungu kwa musaada wake. Walishukuru Bwana kwa kutuma tufani na kushinda adui zao. Walimusifu kwa kupataia Waaskari wa Israeli uwezo wa kushinda. Walimushukuru jinsi alichunga barabara zao na tena watu wanaweza kukusanyika katika vijiji bila woga.

(Kumbusha wanafunzi kama wanapashwa kusifu na kushukuru Mungu wakati anajibu maombi yao. (Zaburi 71:8; 14; Waebrania 13:15)

Debora na Baraka walimaliza wimbo wao kwa ombi hili, “Ee Bwana, tunaomba adui zako zote waangamie. Saidia wanaokupenda kungaa kama jua!”

Taifa la Iaraeli waligeukia Mungu kwa kweli. Waliomba musamaha juu ya kuasi Mungu kwao. Kwa hiyo Mungu hakuendelea kuwaazibu. Muda wa miaka 40, Waisraeli waliishi katika furaha na salama.

Wewe ni mukristo aliyeasi Mungu kwa kutokutii Neno lake? Kama uko na huzuni kweli kuhusu ile na unataka kugeukia Mungu kwa kutubu, atakusamehe na kujaza furaha na salama katika maisha yako.

(**Mwalimu:** Pata muda kwa wanafunzi wako kwa kutafuta ndani ya mioyo yao tabia na hali zinazokuwa kinyume na sheria za Mungu. Uwasukume sana kugeukia Bwana kwa kupata musamaha. Uwakumbushe juu ya azabu ya Mungu kama wakikataa kuacha njia zao za uasi).

SOMO 2 - MWONGOZI WA WAASI (sehemu ya kwanza)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Waamuzi 6:1-32

Shabaa ya somo: Kutimiza kazi yake. Mungu atatumia hata watu wazaifu wanaokuwa tayari.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Bwana anatumika kwa wale wanaomutegemea.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu ya kutumia na Mungu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kufanya mupango wa kusoma Neno la Mungu kila siku, kwa hiyo wataweza kujifunza namna ya kutumiwa na Mungu.
Omba Bwana awasaidie kuongoza waamini wasiotii na waasi kutubu na kufuata Mungu kwa kweli.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Taifa la Israeli linaazibiwa (Waamuzi 6:1-6)
2. Mungu anaharifu Waisraeli (Waamuzi 6:7-10)
3. Mungu anaitwa Gideoni kwa kuongoza taifa lake (Waamuzi 6:25-32)
4. Gideoni anaongoza watu wa Mungu mbali na sanamu (Waamuzi 6:25-32)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti" (Mezali 14:12)

Maelezo kwa mwalimu:

Kisha Baraka na Debora kuokoa taifa la Mungu na Wakanana, Waisraeli waliishi katika salama muda wa miaka 40. Sasa "Walienda vibaya mbele ya macho ya Mungu (Waamuzi 6:1). Kwa hiyo hali (muzunguko) ilirudilia:

1. Waisraeli waliasi Mungu
2. Mungu aliwaazibu
3. Waliomba musamaha
4. Mungu aliwahurumia na kuwapa salama

Kwa wakati ule, azabu ya Mungu ilkuja kwa wale walioishi Midiani. Aliruhusu wawe wakali mbele ya taifa lake. Wakati Waisraeli waligeukia Mungu kwa kuomba musamaha, alivhagua Gideoni kwa kuwaokoa.

Mungu anatumika zaidi kupitia wale wanaokuwa wazaifu. Kwa hiyo, Mungu ndiye anapata utukufu kuliko yule aliyetumia (Tazama 1 Wakorinto 1:26; 31). "Kama Mungu akiwa upande wetu nani atakuwa juu yetu?" (Waroma 8:31). Gideoni alikuwa na uhodari wakati alijua kama Mungu iko pamoja naye. Sukuma wanafunzi wako kujua kama ahadi za Waroma 8:31 ni kwetu leo. Pamoja na kuamini kama Mungu hatatuacha na hatatuachilia, hatuna hitaji tena ya kuogopa juu ya kitu wengine wanaweza kutufanyia (Waebrania 13:5-6).

Tia wanafunzi wako nguvu ya kukata shauri ya namna wanapashwa kutumikia Mungu katika juma linalokuja. Unavuta ili waweze kutegemea Mungu na kuwa na uhodari na ushuja wa kutimiza mipango yao.

Somo: Umekwisha kusema siku moja "Siwezi"wakati mutu mumoja anakuambia ufanye kitru fulani? (Ruhusu wanafunzi wako kupana mifano). Leo tutasikia kitu mutu mumoja, Gideoni alisemaka, "Siwezi kufanya ile." Gideoni alikomalia Israeli wakati Debora alikuwa Mwamuzi. Debora anawakumbusha nini? (Sukuma wanafunzi kuhojeana kuhusu somo la kwanza).

Nyuma ya Mungu kutumia Debora na Baraka, baba yake, na Waisraeli wengine waliishi muda wa miaka 40 katika salama. Kwa mwanzo walitii Mwenyezi Mungu sababu walikumbuka ushindi aliyowapa juu ya adui zao.

Kwa kuendelea, kwa hiyo, kitu kibaya kikatokeya. Wazazi wengi hawakufundisha tena watoto wao kuhusu Mungu wa mbinguni aliye hai. (Tunafahamu kama baba yake na Gideoni aliabudu Bali. Tazama Waamuzi 6:25). Vilevile, taifa la Israeli waliona jirani zao Wakanana wanafurahi na karamu zao za kuabudu mungu wa wa wongo Bali. Baba yake na Gideoni alijenga mazabahu kubwa ambayo jamaa lake na jamii waliweza kutoa sadaka kwa Bali!

Fikiri namna Bwana anajisikia wakati anaona uovu wa Waisraeli. Aliwapenda sana tena sana mpaka alifanya miujiza mingi sana kwa kuwachunga. Lakini hawakumupenda zaidi kwa kumutii. Fikiria ile!

Mambo ilipima kuenda vizuri kwa Waisraeli. Lakini walisahau kitu kimoja. Walisahau kama Mungu muzima anashurtisha utii wa kweli! (Kwa maulizo, fanya mukaguo wa sheria na maonyo ya Mungu. Angalia ingilio ya somo la kwanza).

1. Waisraeli wanapigwa (Waamuzi 6:1-6)

Sawa baba anayependa wana wake, Bwana anapashwa "azibu" (adibisha) taifa lake linaloasi. Kwa wati ule, alichagua kuwaazibu kwa kutumia taifa la Midiani, adui walioishi kusini ya Israeli.

Kwa uangalifu Wamidiani walitazama Waisraeli waliochunga ufugo wao. Walitazama Waisraeli wakipanda mimeya yao.

Onyesha taswira 5: Sasa, wakati mavuno yalikuwa tayari, Wamidiani, waliokuwa wengi sana hata hakuna anayeweza kuwahesabu walipanda ngamia zao na kurukia Israeli. Pale, walikanyaga shamba, waliunguza, kuiba nyama zao na hawakuachia Waisraeli kitu.

Taifa la Israeli, walitazama kutokea mapango ya milima wakiwa na woga. Nyuma, wakati hatari ilipima kuisha, Waisraeli walijitokeza na kuenda kutumika tena katika shamba zao.

Gideoni akapumua, akaambia baba yake, "Sababu gani kupanda tena mimeya? Wakati itakuwa muda wa kuvuna wamidiani watakuja kuiba tena mimeya. Tena kisha kazi zetu zito, hatutapata kitu kwa faida yetu" "Hakose tofauti itkuwa kwa mwaka huu," akasema baba ya Gideoni. "Hakose hawatakuja. Kwa hiyo kama hatupandi kitu, tutakufa na njaa."

Kitu walitumika kwa nguvu. Lakini kwa wakati wa mavuno walipoteza. Mwaka kisha mwaka, katika muda wa miaka 7, wamidiani walifanya uharibifu unaondelea katika shamba za Waisraeli na kupeleka mavuno yote. Walikuwa na nguvu sana hata watu wa Israeli hawangeliweza kuwapiganisha. Maisha gani ya ukosefu waliishi! Ilikuwa tofauti kabisa na yale Mungu alikuwa amepanga kwa taifa lake. (Tazama Torati 8:1). Na yale yote sababu ya mungu aliyetengenezwa na mikono ya watu ambaye waliendelea kuabudu kuliko kusifu Mungu wa mbinguni aliye hai. Walikuwa waasi.

2. Mungu alionya taifa la Israeli (Waamuzi 6:7-10)

Shauri gani wewe ungelipatia Gideoni, baba yake na Waisraeli wengine? (Uwasukume walete majibu. Walipashwa kutubu na kuomba musamaha kwa Mungu muzima ambae majibu yanafikia. Saidia wanafunzi kwa kutja aya za ukarasa ambazo zinapana uhakika kama Bwana anasikia taifa lake wakati wanamurudi. Angalia somo la kwanza, sehemu ya pili).

Mungu alitaka kuokoa taifa lake. Lakini alipashwa kutimiza sababu gani walikuwa na uchafu mingi. Sasa Bwana aliwatumia nabii (muhubiri) pamoja na ujumbe.

Onyesha taswira 6: "Sikia Israeli" akasema nabii: "Nitawaambia sababu gani ninyi ni wenye njaa na wakosefu! Nitawaambia sababu gani Wamidiani wanawatawala na kufanya maisha yenu iwe ya ukosefu! Hamukutii Mungu wa kweli aliye hai! Alitosha taifa lenu toka Misri mahali walikuwa watumwa. Aliwapa inchi hii kusudi muishi ndani yake katika baraka. Aliwaambia, "Mimi ni Mwenyezi Mungu wenu; musiabudu miungu mingine sawa haya mataifa mabaya yanayowazunguka."

"Kuliko kufanya vile, hamukumutii na mulienda mbali naye. Sasa munateswa juu ya uasi wenu."

Nabii alienda mahali pote akihubiri ujumbe huu. Faifa la Mungu lilisikia na kufikiri juu maneno ya nabii.

Gideoni na wengine walitambua kama tumaini lao lilikuwa kurudi kwa Bwana.

3. Mungu aliita Gideoni kuongoza taifa lake (Waamuzi 6:11-24)

Siku moja Gideoni alikuwa akipiga ngano ambayo Wamidiani hawakuongoa. Akiwa na woga wa kutumikia katika njia ya kuingia ndani ya shamba, alipigia ngano katika shinikizo la mvinyo, mahali hakuwa mutu atamwona. (Shinikizo la mvinyo lilikuwa mahali katika shamba ambapo kwa muda wa kuuzisha (mavuno ya mizabibu) mutobe ulikamuliwa na shada kwa kutengeneza mvinyo).

Onyesha taswira 7: Gideoni alikua akifikiri juu ya magumu mazito ya taifa la Israeli. Mara moja, mutu asiyemufahamu akamutokea karibu ya muti uliyokuwa chini yake.

Mbele Gideoni hajasema, mugeni akasema, "Bwana ni pamoja nawe askari wa uwezo na uhodari."

Gideoni akamwambia, "kama Bwana ni pamoja nasi, kwa nini maneno haya yote yametupata?" Hatuna hata chakula cha kutosha kwa kulisha jamaa zetu! Wapi mishangao yote ambayo baba zetu walitupasha? Mungu alipandisha taifa letu toka Misri hadi inchi hii. Sasa ametuacha. Hatujali tena. Aliruhusu Wamidiani watuharibu!

Kisha mugeni akamuambia, "Nitakutuma wewe Gideoni kuokoa Israeli toka mikono ya Wamidiani. Nitakutia nguvu."

"Mimi?" Gideoni alijibu akitetemeka. "Mimi, siwezi kuokoa Israeli. Jamaa yangu ni masikini na mimi niko mutu mudogo katika jamaa langu. Siwezi kamwe kuikoa Israeli toka Wamidiani. Hapana, utatafuta mwengine. Siwezi kufanya hivyo!"

"Usiwe na woga. Nitakuwa pamoja nawe. Nitakutia nguvu. Nitakusaidia kuharibu Wamidiani."

Gideoni akajiuliza: Ni kweli malaika wa Bwana?

Akageukia mugeni, Gideoni akasema, "Kama nimepata neema machoni pako, tafazali unionyeshe alama kama wewe ni Bwana. Usiondoke hapa ninakuomba hata wakati nitakapokuja kwako nitoe zawadi yangu na kuiweka mbele yako."

"Nitakungoja" akasema malaika aliwachunga.

Wakati Gideoni aliporudi malaika wa Bwana alimuonyesha jiwe kubwa akamuambia, "Tia nyama na mukate juu ya mwamba (Jiwe kubwa). Mwanga muchuzi juu ya mwamba."

Gideoni akatii. Kiisha malaika akagusa chakula na incha ya fimbo (gongo) yake. Gafula moto uikawaka na kuteketeza nyama na mukate juu ya mwamba. Kwa wakati ule malaika akapotea.

Gideoni aliogopeshwa. Akasema: "Ole kwangu, Ee Bwana Mungu! Kwa kuwa nimeona malaika wa Bwana kwa macho." Gideoni aliogopa sababu alifikiri kama atakufa (angalia Kutoka 33:20).

Bwana akamutia moyo akisema, "Usiogope. Hautakufa." (Linganisha na Yoshua 5:13-15).

4. Gideoni aliongoza taifa la Mungu mbali na Mungu (Waamuzi 6:25-32).

Kwa usiku ule ule Mungu alimuruhusu, "Gideoni; bomoa mazabahu baba yako alijengea Bali!"

Gideoni akasema, taifa lote linaabudu Bali kwa mazabahu hii. Nikiibomoa wataniua!

Bwana akaendelea, "Kisha kubomoa mazabahu ya Bali, uharibu vitu vya dini vinavyokua juu ya mazabahu. Kisha unijengee mazabahu. Angusha miungu ya miti na weka makuni yake juu ya mazabahu yangu. Kamata ngombe dume katika kundi la baba yako, na umutoe sadaka kwa ajili yangu.

Kwa wakati huu Gideoni hakusema tena, "Mimi siwezi!" kwa Mungu. Alikuwa tayari kutii. Lakini alikuwa na woga: aliogopa jamaa yake, aliogopa watu wa inchi yake.

Vilevile kwa usiku ule hapana muchana, Gideoni alikamata wanaume kumi kwa kumusaidia kutii sheria za Mungu.

Namna gani unawaza, wanaoabudu Bali walifanya nini wakati waliona mazabahu yao imeangushwa? (Acha wanafunzi wapane mawazo yao).

Onyesha taswira 8: "Nani aliyefanya hivi?" Walisema na hasira.

"Bali atakasirika juu yetu. Atatuazibu!" wakanungunika.

Wakati walipojua kama ni Gideoni aliyebomoa mungu wao, kundi la watu wakaenda kwa baba yake na Gideoni wakisema, "Tunahitajio Gideoni. Anapashwa kufa. Alibomoa mazabahu yetu na kuangusha miungu yetu. Umulete kusudi tupate kumuua!"

Akanyanyua mikono yake juu kwa kunyamazisha watu, baba yake naGideoni akasema, “Munisikilize! Hamuna haja ya kuazibu Gideoni. Muache Bali amuazibu, kama Bali ni Mungu, hana haja ya musaada wenu. Ajisimamie na kuazibu yule aliyebomoa mazabahu yake! Ni ujinga kwenu kufikiri kama anahitaji musaada wenu!” (Mwalimu: Sisitiza kama mungu asiyeweza kujiokoa mwenyewe hapashwi kuabudiwa).

“Ni kweli, wakasema wale wanaoabudu Bali. “Wakati Waisraeli watakapoona yale Bali atafanyia Gideoni, watajua kama Bali ni mungu pekee anayepashwa kuabudiwa.”

Kisha walichunga na kuchunga tena. Nini itafanyika (Hakuna kitu). Sababu gani? (mungu-sanamu) ni kitu kisichokua na faida. Sanamu haiwezi kamwe kufanya kitu. (Angalia Zaburi 135:15-17)

Sababu Bali hakuweza kusaidia watu, walikuwa tayari kufuata Gideoni mwongozi wao? Tutapata jibu kwa ile ulizo kwa mukutano ujao.

Tunaweza kupata mafundisho gani toka Gideoni? (furahia majibu ya wanafunzi. Haiwezekani andika mawazo mamoja kwa ubao). Kwa mufano:

1. Kwa kazi yake, kwa kawaida Mungu anatumia hata watu wazaifu, watu wanaomutegemea na kumutii. Anaweza kukitumia wewe na mimi.

2. Gideoni alitegemea ahadi ya Mungu kwa kupata nguvu na musaada. Wakati Bwana anatuomba kufanya kitu fulani kwa ajili yake, tunakuwa na ahadi ya nguvu yake pahali pa uzaifu wake (2 Wakorinto 12:9-10).

3. Hata kama Gideoni aliogopa, alitii Mungu (Soma Matendo 5:29 na Waroma 8:31) kwa sauti kubwa.

4. Bwana akaheshimu Gideoni kwa musimamo aliyokuwa nayo. (Soma ahadi ya Mungu kwetu katika Yoane 12:26).

Sijuwe namna gani Mungu anataka kukutumia. Lakini ninajua kama anataka kila mumoja wa watoto wake awe tayari na hamu ya kumutumikia. (Anglia Waroma 12:1-2; linganisha na 1 Wakorinto 6:19-20).

Kwa kazi yake, Bwana anachagua kila mara watu wadogo kusudi Mungu apokee utukufu kwa yale yaliyotimizwa (Angalia 1 Wakorinto 1:26-31).

Uliza Mungu akuonyeshe namna gani na pahali gani atakutumia juma hili. Unajua mukristo ao mwamini asiyetii Mungu wa mbinguni mbele ao nyuma. Ni wakati tu muasi anatubu na kutafuta musamaha wa Mungu anataka uongoze muasi mumoja kwake. Kama amechagua kukutumia, umuombe bidii ya kufanya kazi yake. Kama vile Gideoni alikuwa, wewe unahitaji kufanya mapenzi ya Mungu? Kama ni vile, Mungu atakupa nguvu ya kufanya hata kazi yake kubwa.

SOMO 3 - MUONGOZI WA WAASI (sehemu ya pili)

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Waamuzi 6:33 – 8:32
Shabaa ya somo: Onyesha kama uwezo wa Mungu unaweza kutusaidia katika kila matokeo ya maisha yetu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Mungu anatulinda. Anataka tumuwekee tumaini na tusiogope.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Tumaini inayotegemea Mungu.
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuweka kwa ufahamu Zaburi 56:3 ao sehemu hii ya Isaya 12:2: "Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu; nitatumaini, na sitaogopa."

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Gideoni anakosa tumaini kwa Mungu (Waamuzi 6:33-40)
2. Mungu alichagua jeshi la Gideoni (Waamuzi 7:1-6)
3. Mungu anapatia Gideoni imani (Waamuzi 7:7-15)
4. Mungu anapatia jeshi la Gideni ushindi (Waamuzi 7:16:23)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Kuna njia inayoonekana kuwa sawa kwa macho ya mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti" Mezali 14:12

Maelezo kwa mwalimu:

Fanya mukaguo na mazungumuzo (hali) ya Waisraeli
1. Waisraeli waliasi Mungu
2. Mungu aliwaazibu
3. Waliomba Musamaha
4. Mungu aliwasamehe na kuwapa salama.

Hakikisha kama Mungu alikuwa tena tayari kuwasamehe watu wakati walitubu kwa kweli.

Kwa utumishi wake, Mungu anahitaji watu wanaojaa imani na hapana woga. Shetani anasukuma mara nyingi waamini kujiuliza kama wako katika mapenzi ya Mungu ao hapana. Wanakuwa kama Gideoni aliyekuwa na magumu haya: Imani yake haikuwa imara. Mara nyingi hakuwa na uhakika; kwa wakati mwingine alikuwa na tumaini ya kweli kwa Mungu. Tunaona uvumilivu na Mungu kwa alama za kufuatana alizopana kwa Gideoni kwa kutia imani yake nguvu.

Wakati Gideoni alitegemea Mungu kwa kweli, aliona Mungu akifanya miujiza mukubwa kwa Waisraeli, kuwasaidia kwa adui zao Wamidiani.

Ukosefu wa imani ni mwanzo wa woga. (Angalia 1 Yoane 4:18). Woga wetu unatuzuiya kuwa na mafaa kwa Mungu. Zaburi 56:3 ao Isaya 12:2) ni dawa. Omba Mungu akusaidie kumuamini katika kila hali.

Somo: Munakumbuka kazi ya nguvu ambayo Mungu alipatia Gideoni? (**Mwalimu:** angalia tena somo la 2, sehemu ya 4. Onyesha kama kila mara fasi ya nguvu zaidi kwa kutumikia Mungu ni ndani na inje ya nyumba yetu).

Gideoni alikuwa na uhodari wa kubomoa mazabahu ya Bali, aliamini kama Mungu alimuamuru kufanya hivi. Na alitegemea Mungu kusudi amusaidie.

1. Gideoni anakosa kutumainia Mungu (Waamuzi 7:1-6)

Ilikuwa ingali muda wa mavuno katika Israeli: kila mwanainchi alitumaini kama Wamidiani hawataiba tena mavuno yao kwa mwaka ule.

Lakini waliona! Jeshi lao liliendela kuwa likubwa zaidi! Waadui wengine wa Waisraeli walijiunga na Wamidiani mara hiyo. Kwa jumla kulikuwa na zaidi ya waaskari 135,000 (angalia Waamuzi 8:10).

Waisraeli walijisemesha, "Tutapoteza tena mavuno yetu! Tutafanya nini? Nani anaweza kutusaidia?"

Lakini nini Bwana aliambia Gideoni wakati alikuwa akipiga ngano karibu na shinikizo? (Kagua somo la 2, sehemu ya 2). Sasa ilikuwa muda wa kutenda!

Gideoni alituma wajumbe kwa waaskari wote wa Israeli. "Muje mujiunge nami. Tutapiganisha adui zetu!" watu wote wa Israeli walisikia yale Gideoni alikuwa akisema. Mara moja waaskari 32,000 walijibu.

Kwa wakati ule Gideoni alipoteza uhodari. Aliwaza, "Ninatumaini kama ninaweza kuwa na uhakika kama Mungu anataka mimi niongoze jeshi kwa kupiganisha adui zetu."

Unawaza kama Mungu atafanya ile aliyoahidi ku shinikizo wakati aliahidi Gideoni kushinda Wamidiani? (alituma moto iliyounguza nyama na mkate).

Sasa, pahali awe na tumaini kamili kwa Mungu, Gideoni alimuomba tena alama ingine. "Ee, Mungu!" Akaomba, "kama utanitumia kuokoa taifa langu, unionyeshe ikikupendeza. Nitatia uongozi wa kondoo chini usiku. Kesho asubui, kama inchi inayoizunguka ni kavu na ngozi analowana na umande, nitatambua sasa kama utanisaidia."

(**Mwalimu:** Eleza kama ngozi hii ni nguo inayotengenezwa na manyoo ya nyama. Kama hiyo haiko wazi, tumia nguo inayoweza kukunywa maji kwa kuonyesha mufano wa alama ya Gideoni).

Sababu gani, ee ni sababu gani Gideoni alikuwa akiuliza Mungu wa mbingu na dunia?

<u>Onyesha Taswira 9</u>: Kesho yake asubui Gideoni alienda kuangalia ngozi. Unawaza alikuta nini? (Acha wanafunzi wajibu. Soma Waamuzi 6:38). Alikamata ngozi na ikatoa maji ya kujaza bakuli.

Gideoni alipashwa kufanya nini? (Muulizane. Kuamini Mungu na kutenda).

Ole, Gideoni hakuendelea kuamini Mungu. "Ee Mungu," akaomba, "Ikipendeza, kasirani yako isiwake kwa ajili yangu. Nipatie tena alama. Usiku huu tena nitatia ngozi. Mara hii, fanya inchi kavu iwe na umande na ngozi isiwe na maji. Sasa sitakuwa tena nwa woga wa kupiganisha jeshi kubwa la wamidiani."

Unawaza nini Gideoni alikuta asubui? (Acha wanafunzi wajibu. Soma Waamuzi 6:40). Alikuta ngozi inakauka sana, ikizungukwa na udongo (inchi kavu) inayoloana na umande.

Ni kwa uvumiliovu gani Mungu alijibu maombi ya Gideoni! Kuliko Gideoni awe na woga, Gideoni alitegemea tu Mungu.

2. Mungu alichagua jeshi la Gideoni (Waamuzi 7:1-6)

Kwa mwisho, alitumaini kama Mungu alikuwa pamoja naye, Gideoni aliongoza jeshi lake la watu 32,000 hadi milima inayozunguka kampi ya Wamidiani. Waaskari wa Israeli walitazama adui zao waliokuwa bondeni. Waaskari wa Israeli waliwaza, "Hili ni jeshi gani!" Wamidiani wanakuwa na jeshi kubwa mara ine kuliko yetu na ngamia nyingi zisizohesabiliwa (Angalia Waamuzi 7:12).

Mungu alisema kwa Gideoni, "Gideoni, uko na watu wengi katika jeshi lako."

Gideoni aliwaza, zaidi! Jeshi letu ni ndogo zaidi kuliko ya Wamidiani!

Mungu alifahamu lile Gideoni aliwaza. "Kama ukipiga Wamidiani na jeshi hili kubwa, taifa lako watafikiri ni wao wenyewe wamefanya vile", Mungu akasema "Nyuma ya vita, ninataka wakumbuke kama ni mimi niliyewapa ushindi."

Mungu akaeleza namna gani Gideoni anapashwa kupunguza jeshi lake. Kufuatana na maagizo ya Mungu Gideoni akawaambia watu wake, "Kila mutu anayeona woga wa kupigana ataacha na kurudi nyumbani!"

Gideoni aliogopa wakati aliona watu wake wanamuacha kwa mia na elfu! Ilionekana kama vile jeshi lake lote linarudi. Jumla ya watu 22.000 walirudi nyumbani! Sasa ni watu 10,000 tu wanabaki.

Gideoni akaambia Mungu kuhusu ukubwa wa jeshi lake. Uliniambia niache waaskari wanaoogopa. Sasa ninakuwa tu na watu 10,000 kwa kupiganisha jeshi kubwa la Wamidiani katika bonde. Ile haiwekane!"

Mungu akajibu, "Hata hivi ungali na watu wengi katika jeshi lako."

Wengi zaidi! Aliwaza Gideoni. Jeshi la Wamidiani linakuwa na zaidi ya mia na mia kuliko sisi.

Mungu akaamuru, "Paleka watu wako ngambo ya muto na uwachunguze wanapokunywa maji." Gideoni alitii.

Onyesha taswira 10: Wengi wa watu walitia mara moja vinywa vyao ndani ya maji na kunywa. Lakini askari zao walishota maji na mikono. Waliitia ndani ya vinywa na kama imbwa wanaoramba, waliangalia ngambo na ngambo kama adui anaweza kutokea.

"Gideoni, na watu wake 300 walienda kushinda Wamidiani," aliahidi Mungu. "Tuma wengine nyumbani mwao."

Gideoni hakukataa tena, alifahamu kama Mungu aliyemupataia kwa uvumilivu alama tatu aliweza kusaidia Waisraeli na adui zao. (Kagua (angalia tena) alama : Moto uliyounguza chakula, alama mbili na ngozi). Sasa, kwa mmwisho, Gideoni anatii Mungu kwa kweli.

3. Mungu alipatia Gideoni imani (Waamuzi 7:7-15)

Namna gani unaweza kujisikia kama ungelikuwa ku fasi ya Gideoni? Alikuwa na watu 300 wasiokua na ujuzi wa kupiganisha watu 135,000 waliofungwa vizuri; waaskari. (Muzungumuze pamoja. Onyesha kama mutu asiyejulikana anatuletea woga mara kwa mara hata kama tunaamini Mungu).

Gideoni alifahamu kama Mungu aliahidi kuokoa Waisraeli toka adui zao. Lakini hakujua namna gani ataitimiza. Mungu alijua kama Gideoni alikuwa na woga. (mwalimu: kazia juu ya uwezo wote wa Mungu).

Usiku ule Mungu akasema, "Gideoni, wakati utakuwa na woga, kamata mutumishi wako na njiingize ndani ya kampi ya Wamidiani. Wakati utasikia wanayoyasema hautakuwa na woga muda murefu. Kuliko kufanya vile ujiharikikishe kuwashambulia.

Mbele hata kama Gideoni alikuwa hajauliza sababu ya ile, Mungu alileta alama ingine kwa mutu huyu ambae hakutegemea Mungu kwa kweli. Ni kwa upendo na uvumilivu gani Mungu anatia nguvu munyonge na muzaifu Gideoni!

Alienda katika giza, Gideoni na mutumishi wake walifika karibu na njia inayoenda kwa kampi ya Wamidiani. Kundi la Waaskari lilifunika bonde lote.

Onyesha taswira 11: Mara moja, Gideoni na mutumishi wake waksikia mutu akasema. Kwa kupumua, waliweka masikio yao karibu na hema kwa kusikia vizuri.

Moja wa waaskari alikuwa akisema, "Nikiota ndoto ya kigeni. Mukate wa shairi ulianguka katikati ya jeshi la Midiani. Ulifika kwa hema yetu na kuiangusha.

Askari mwengine akafasiria, "inaweza kumaanisha kitu kimoja. Gideoni iko anaongoza waaskari wamoja kwa kutupiganisha. Atashinda sababu Mungu iko pamoja naye!"

Unawaza Gideoni alijisikia namna gani wakati alisikia vile? (Muzungumze. Soma Waamuzi 7:15. Gideoni alishukuru Mungu, alijiharikisha kushambulia Wamidiani, alikuwa muhodari).

(Mwalimu: Kazia juu ya muda muzuri wa Mungu katika tukio lile. Hata kwa siku zetu, Mungu anaruhusu maneno kwa kuhakikisha uongozi wake katika maisha yetu).

4. Mungu anapana ushindi kwa jeshi la Gideoni (Waamuzi 7:7-15)

Aliporudi haraka kwa watu wake, alisema, "Muamuke! Usiku wa leo Mungu anatupa ushindi juu ya Wamidiani."

Waaskari 300 walisikiliza. Gideoni alipatia kila askari baragumu, mutungi mutupu na mienge ya moto. Silaha gani za kigeni! Lakini Gideoni alifuata maongozi ya Mungu. Njia za Mungu ni juu ya njia zetu (Angalia Isaya 55:8-9).

Mutie mienge yenu ndani ya mitungi", Gideoni akaamuru. "Tutashambulia Wamidiani wakati wanalala. Musifanye fujo! Hatutaki mutu atusikie ao kutuona hivi tunakaribia kampi yao."

Kisha Gideoni akaagiza waaskari 100, "Mujipange karibu na kampi." Kwa kundi lingine la 100, aliwaamuru, "Mwende ngambo ingine ya kampi" "Muingie nyuma ya kampi", akaambia wengine 100.

“Munifuate na mufanye ninalolifanya” Gideoni akaagiza. “Nitakapopiga baragumu, mutapiga zenu na mara moja muvunje mitungi yenu. Kisha muweke mienge yenu juu na kulalamika,” “Upanga wa Bwana na wa Gideoni.”

Nyuma katika usiku, watu wa Israeli walijipanga polepole. Kila kitu kilikuwa kimya katika kampi ya Wamidiani. Kwa muda wa miaka sabak, walikuja katika Israeli na kukamata mambo yote walitaka. Sasa, walikuwa tayari kufanya vile tena. Hakuna mutu katika jeshi la Wamidiani aliyekuwa na woga ila yule askari aliyekuwa na ndoto pamoja na rafiki yake!

Mara moja vikosi vya Wamidiani viliamuka juu ya baragumu. Ikawa fujo kubwa!

Onyesha taswira 12: Watu wa Midiani walikimbia inje ya hema zao. Katika mustuko wao, walizungukwa na moto wa mienge! Walisikia watu wakilalamika, “Upanga wa Bwana na wa Gideoni!”

Walifikiri wanashambuliwa na jeshi kubwa, waaskari wa Wamidiani waliogopa. Pahali pa kupigana walikimbia. Hapakuwa njia ya k ukimbilia kwa kuponyoka na kuenda kwa inchi yao. Katika uvuguvugu wao, Wamidiani walianza kupigana na kuuawa wao wenyewe.

Gideoni na watu wake waliwafuata na kuharibu jeshi lote la Wamidiani! Walipopata ushindi huu wa kimujiza, waisraeli walitaka kufanya Gideoni mufalme wao. Lakini Gideoni alikataa “Hapana, siwezi kutawala juu yenu. Hakuna hata mumoja wa watoto wangu atakayetawala. MUNGU ATAKAYETAWALA JUU YENU! Ni yeye alitupa ushindi.” Gideoni akakumbuka haya jinsi alikuwa muzaifu na mwenye woga.

Nyuma ya kupigana, Gideoni aliishi tena muda wa miaka 40. Na Waisraeli waliishi katika salama, salama pamoja na Mungu na katika salama na wengine. Hakuna hata adui mumoja aliyewazuru.

Bwana anajua kama matakio mamoja mamoja yanatutia woga. Ndio maana anatuambia tumutegemee kuliko kuwa na woga. (Saidia wanafunzi wako kufahamu Zaburi 56:3 ao sehemu ya kwanza ya Isaya 12:2).

Mungu wa kweli na aliye hai aliyesaidia Gideoni ni yeye anayeahidi kutusaidia (Waebrania 13:56-6,8). Angalia tena muzunguko wa historia ya Israeli muda wa siku hizi. (Onyesha taswira ndani ya jalada ya mwisho).

1. Waisraeli walienda mbali na Mungu (waliasi)
2. Kwa kuazibu taifa la Israeli, Mungu alitumia adui zao
3. Walitubu na kuomba Mungu musamaha
4. Mungu aliinua mwamuzi kwa kusaidia Waisraeli, aliwasamehe na kurudisha salama katika inchi.

Hakikisha kama Bwana hatumie njia moja tu kwa kutimiza ahadi zake. Kwa kusaidia Debora na Baraka, alitumia mvua. Alituma uvuguvugu kwa kusaidia Gideoni.

Leo vilevile, Bwana Mungu anatumika kitofauti na kila mwamini kwa kumuongoza na kumusaidia.

SOMO 4 - SAMUSONI ANAASI

Kwa mwalimu kujifunza mbele: Waamuzi 13:16

Shabaa ya somo: Ni kuonyesha kama huzuni na musiba ni matokeo ya kuasi Mungu
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Uasi unaleta huzuni na kushindwa
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Hamu kubwa ni kupendeza Mungu tu
Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Kuchunguza katika maisha yao kila hali ya uasi na kutubu.

Somo kwa kifupi: (kuandika ndani ya buku ya mwalimu na za wanafunzi.)
1. Wafilistini, adui za Israeli (Waamuzi 13:1; 1 Samweli 31:9; 2 Samweli 5:21)
2. Wazazi wa Samusoni (Waamuzi 13:1-25)
3. Manisha ya uasi ya Samusoni (Waamuzi 14:1-6:20)
4. Kifo cha Samusoni (Waamuzi 16:21-31)

Shairi la kujua kwa ufahamu: "Kuna njia inayokuwa sawa kwa macho ya mutu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." (Mezali 14:12)

Maelezo kwa mwalimu:

Nyuma ya Gideoni Waisraeli waliendelea na hali yao ya uasi, azabu, kutubu, musamaha na salama. (Angalia taswira ngambo ingine ya jalada ya mwisho). Waliposahau huruma ya Mungu na maonyo yaike kwao, "wana wa Israeli walifanya tena mambo yasiyopendeza Mungu" (Waamuzi 13:1). Kwa wakati ule, Mungu aliazibu taifa kupitia Wafilistini muda wa miaka 40.

Mungu alikusudia kusaidia Waisraeli kupitia mwamuzi Samusoni. Mungu alipatia Samusoni nguvu zisizokuwa za kawaida ambazo zilipashwa kutumiwa kwa ajili ya bwana. Kwa hiyo, sababu ya hitaji baya ya Samusoni kwa kuendea zambi, alichelewa katika kusaidia Waisraeli toka Wafilistini. Pahali pa kuwa muongozi kama vile ilipashwa, aliasi Bwana. Ile ikamuletea uharibifu.

Agiza na tia mukazo kwa wanafunzi wako juu ya hatari ya kuasi Mungu. Hata kijana anapashwa kufunzwa hatari ya kufuata na kuoa wasioamini. Maisha ya Samusoni ni mufano wa kweli kwa uchungu na magumu ya kuoa asiyeamini. (Angalia Amosi 3:3; 1 Wakorinto 7:39; 2 Wakorinto 6:14).

Leta mali kidogo katika somo na nunua kitu kidogo kwa wanafunzi. Onyesha waziwazi kama kitu kilichonunuliwa ni kwenu sasa. Sababu ulipana mali kwa ajili ya kile kitu, munaweza kukitumia namna mnapenda.

Soma basi 1 Wakorinto 6:19-20. Hakikisha kama Wakristo walikombolewa kwa damu ya Samani ya Bwana wetu Yesu Kristo. Vilevile, yeye mwenyewe ana uwezo wa kututumia kwa ajili yake jinsi atakavyo. Kupendeza Mungu si jambo la uchaguzi wetu lakini ni tendo la ukombozi wa Kristo peke yake. Utii unapendeza Bwana. Anapashwa kuadibisha wanomuasi. Chunga, uonyeshe kweli hizi katika moyo wa wanafunzi wako wakati unafundisha uchungu wa maisha ya Samusoni.

Kwa kukagua yale uliyofundisha katika masomo yaliyopita, chagua wanafunzi watatu mbele ya kuanza somo, mumoja atakua Debora, mwengine Baraka na watatu Gideoni. Uwaruhusu kusema kwa ufupi namna gani Mungu alitumia hawa watatu kwa kusaidia Waisraeli toka adui zao. Kagua hali ya uasi (kuenda mbali na Mungu). Tumia taswira (kwa jalada ya mwisho) kwa kuonyesha hali ya uasi, azabu, kutubu, musamaha na salama.

Mbele ya kuingia kwa masomo funika taswira 15b.

Somo:

1. Wafilistini adui za Waisraeli (Waamuzi 13:1; 1 Samweli 31:9; 2 Samweli 5:21)

Tungeliwaza kama nyuma ya misaada yote Bwana Mungu alileta kwa waisraeli, wangeliendelea kushukuru na kutii Mungu. Lakini! Walienda mbali naye mara tena. Hawakutii kwa njia ya kuungana na mataifa za wapagani waliowazunguka na kuabudu sanamu. Kwa wakati ule Mungu aliazibu Waisraeli kwa kuruhusu Wafilistini wawatawale.

Wafilistini walikua watu wa dini lakini waliweka imani yao katika dini ya uongo. Moja kati ya miungu yao iliitwa Dagoni. Sanamu hii ilikuwa na sura na viungo vya mutu wa mwili wa samaki.

Jeshi la Wafilistini lilipigana na mikuki na panga za chuma. Waaskari wa Israeli walikuwa na silaha za miti. Muda wa miaka 40 Wafilistini walifanya mazoezi yao ya kiaskari katika vijiji vya Israeli.

Onyesha taswira 13: Wafilistini hawakuiba tu, walikamata vijana kama watumwa.

Kwa nini Mungu aliruhusu ile?

2. Wazazi wa Samusoni (Waamuzi 13:1-25.)

Katika kijiji ndogo ya vilima Sora katika Israeli, kuliishi Manoa na muke wake. Wale wawili walipenda Mungu na walimuabudu. Ile alifanya Manoa na muke wake wanakasirika kuona watu wanainama mbele ya sanamu.

Walishushwa moyo sana sababu hawakuwa na watoto. Hata vile walitegemea Mungu na kumutumikia.

Siku moja malaika alitokea muke wa Manoa na kumuambia, "Umechunga muda murefu kupata mutoto. Sasa sikiliza: Bwana atakupa mutoto!

Malaika akaendelea, "Ongoza kijana wako kwa Mungu. Wewe na mutoto hakuna atakayekunywa mvinyo. Usikate nyele zake. Mungu anataka mutoto wako awe munaziri kwa Mungu. Bwana atamutumia kwa kuokoa taifa la Israeli na Wafilistini."

(Mwalimu: Fasiria kama mutu anayewekwa kwa Mungu anaitwa munaziri. Angalia Hesabu 6).

Muke wa Manoa alikimbia kwa mume wake kwa kumuelezea habari hii ya ajabu.

Onyesha taswira 14: Manoa akainama kichwa chake na kuomba: "Ee Bwana, ikikupendeza ututumie tena mujumbe wako kwa kutufundisha namna gani tutafanya na mutoto wako." (Mwalimu: Kazisha baraka ya kuona wazazi wanaomba Bwana hekima ya kukomalisha watoto wao. Sukuma wanafunzi wawe na shukrani na watiifu kwa wazazi wa namna hii. Kwa kufanya hivi, watapendeza Bwana).

Mungu akajibu maombi ya Manoa na kumutumia tena malaika kwa kurudilia maagizo. Kisha Manoa alitoa sadaka ya mwana mbuzi na mukate kwa Mungu. Kama vile moto na moshi ilipanda mbinguni, ndivyo malaika alipanda mbinguni kwa muda ule ule. Manoa na muke wake wakaanguka kifudifudi udongoni sababu walifahamu kama mujumbe alikuwa malaika wa Mungu. Wale wawili walipendeza Mungu kwa kuamini ahadi yake. Wakati mutoto alizaliwa walimupa jina la Samusoni. Walimuangalia akikomaa na walijua kama Mungu amemubariki.

3. Maisha ya uasi ya Samusoni (Waamuzi 14:1-6:20)

Biblia haituambie kitu juu ya utoto wa Samusoni. Kama watoto wote, aliuliza maulizo mengi. Ile inaweza kufanana na kitu kama kile kwake…

"Baba, sababu gani siwezi kuwa na nyele za kunyolewa sawa na vijana wengine?"

"Samusoni, mbele ya kuzaliwa kwako, Mungu alisema kama wenbe usipite juu ya kichwa chako. Alisema iko na kazi maalumu ya kukupatia. Utaokoa taifa la Israeli toka wafilistini waovu ambao ni wabaya kwetu", baba yake akajibu.

"Namna gani nitafanya vile?" Samusoni akauliza.

"Sijui mutoto wangu. Mungu atakuonyesha. Sasa unapashwa kumutii. Usinyoe nyeloe zako hata siku moja na usikunywe mvinyo."

Wakati Samusoni alikuwa kijana, aliona katika Timuna muji wa karibu na Filistini, musichana muremmbo. Aliporudi kwao, akaambia wazazi wake, "Nimependa musichana wa Filistini. Nataka munioeye yule musichana!" (Kwa wakati ule, wazazi walimuoea katika inchi ile).

"Binti yule hakuamini Mungu. Aliabudu sanamu. Sababu gani haukuoa muIsraeli? Mama yake akamusihi.

Baba yake akamukumbusha, "Mungu alikataza taifa lake kuoa (ao kuolewa) wapagani wasioamini (Torati 7:3). Tena wafilistini ni adui zetu!" Samusoni anakumbuka tena kama aliwekwa wakfu kwa Mungu kwa kuokoa Waisraeli toka Wafilistini?

Samusoni alikataa kusikiliza wazazi wake. "Huyu binti anamipendeza. Na ninamutaka kama muke wangu." Alijibu na kiburi. Alijua jinzi Mungu alitaka awe na afanye. Lakini hakujali na ile. Alitaka kufuata njia yake mwenyewe. Kwa kutaka njia yake na kuacha ya Mungu, ni uasi.

Katika njia ya kuenda Timuna kwa natayarisho ya ndoa, Samusoni alishambuliwa na simba. Kwa wakati ule Bwana alipatia Samusoni nguvu zisizokua za kawaida za kuua simba na mikono yake tu. Hakusema kitu kuhusu hili jambo kwa wazazi wake ao mutu mwengine.

Nyuma kidogo, wakati alienda Timuna juu ya ndoa, alienda kuangalia kama maiti ya simba ingali pale. Ilikuwa pale na ndani yake kulikuwa kundi ya nyuki na asali. Samusoni alikamata asali katika mikono yake na akatoka akikula katika njia. Alipatia baba yake na mama yake. Lakini hakuwaaombia namna gani asali hii ilipatikana. Ilikatazwa kwa munaziri kugusa maiti.

Nyuma ya ndoa pale Timuna, Samusoni alifanya karamu iliyodumu siku saba.

Kwa mwanzo wa karamu, Samusoni aliambia rafiki zake 30. "Nitawaambia fumbo. Kama mtanifasiria katika siku hizi siku 7 nitawapa ninyi nguo za kitani 30."

"Sawa! Utuambie fumbo," rafiki wakasema.

"Katika mwenye kula chakula kinatoka chakula, na katika mwenye nguvu unatoka utamu." Samusoni alisema juu ya simba na asali.

Vijana walifikiri na kufikiri tena. Hawakuweza kuleta maana ya fumbo mbele ya ndoa. Katika uchungu na kazirani waliendea muke wa Samusoni na kumuambia, "Kama hautuambie fumbo la Samusoni tutakuunguza wewe na nyumba ya baba yako!"

Akaendea Samusoni, akamuambia, "Sababu gani hauniambie maana ya fumbo lako?"

"Sikusema kitu kwa wazazi wangu. Sababu gani nikuambie?"

"Haunipendi!" akalia. "Ungelinipenda ungeniambia maana."

Siku nyuma ya siku, alijisemesha kwa kumwambia amupe maana. Kwa mwisho, kwa siku ya saba Samusoni alimupa maana. Unawaza nini muke wa Samusoni alifanya wakati alipata maana ya fumbo? (Acha wanafunzi wajibu. Soma Waamuzi 14:17)

Aliambia wale Wafilistini 30 maana. Wakakimbilia Samusoni wakimuletea jibu. Kisha alipatia kila mutu nguo za kitani.

Kwa kulipa deni yake, Samsoni akaenda katika mji mwengine wa Filistini, akaua watu 30, na kukamata nguo zao kwa kupatia waalikwa wake wa Timura. Alikuwa na kasirani ya kuacha muke na kuenda kuishi na wazazi wake. (Kwa hiyo tunaona kama alichagua vibaya, kuoa muke aliyekatazwa na wazazi na sheria ya Mungu).

Alipashwa kubaki nyumbani. Pahali pa kubakia, aliamua kuenda kuangalia muke wake. Wakati alipofika Timuna, akasikia kama muke wake ameolewa tena na mutu mwengine. Samusoni alikasirika sana hadi akachoma moto mashamba ya Wafilistini na kuua watu wengi. Kwa mwisho alianza kufanya kazi kwa kushinda adui, lakini si kwa sababu zuri.

Sasa Wafilistini walikuwa na hasira: kuua Samusoni. Jeshi lao likatembea juu ya Israeli.

Walilalamika, "Tunataka Samusoni. Mumulete ao tutawaua!"

Wanaume elfu tatu (3,000) ya waIsraeli walienda kwa Samusoni. "Umetufanyia nini?" Wakamuuliza. "Tunakuja kukufunga na kukupana. Kama hatufanye vile, watatuua."

Kisha Samusoni akawaruhusu wanufunge na kamba nyipya na kumutoa kwa adui zake. Waaskari wa Filistini wakafurahi sana. Sasa walipashwa kulipiza kisasi kwa mutu huyu.

Lakini Roho wa Bwana alikuja na ushindi juu ya Samusoni, akamutia nguvu nyingi sana. Alikata kamba sawa vile nyuzi ya kitani inayoungua.

Onyesha taswira 15 (ficha taswira 15b): Aliona mufupa wa taya ya ngamia, Samusoni akaikamata na kuua Waaskari 1,000 wa Filistini. Mara tena, Samusoni alitimiza mupango wa Mungu kwake kwa kuokoa Waisraeli na Wafilistini.

Aliporudi nyumbani, watu walimukaribisha kama shujaa na wakamufanya kuwa mwamuzi (Kiongozi). Muda wa miaka 20 Samusoni aliongoza Israeli kwa musaada wa Mungu.

Lakini Wafilistini walimuchukia na walichunga muda wa kumukamata.

Usiku moja Samusoni alishuka katika muji wa Filistini unaoitwa Gaza. Wakati wakubwa wa muji walimuona waliambia waaskari wote na walinzi. "Samusoni iko katika muji", walilalamika. "Musimuache akimbie. Muzunguke muji. Muchana kati tutamuua! Usiku kati, Samusoni aliamuka, akashika milango ya lango la muji na nguzo zake mbili, pamoja na kipingo. Akazitia kwa mabega yake, akazibeba juu ya mulima wa Israeli umbali wa kilometa 63.

Wafilistini walikasirika. Hawakukamata Samusoni na sasa walipashwa kutengeneza milango mingine ya muji!

Sawa vile Mungu alikuwa akimusaidia mara nyingi, unafikiri kama Samusoni alipashwa tu kutii Mungu. Kuliko kufanya vile, alianguka katika mapenzi na muke Mufilistini aliyeitwa Delila. (Angalia tena Torati 7:3. Matokeo ya Timuna haikufundisha Samusoni kitu).

Wakubwa wa Wafilistini waliahidi mali nyingi kwa Delila kama angeliweza kufahamu asili ya nguvu za Samusoni. Kwa kufanya vile, Delila alijifanya mupendwa wa Samusoni. Alimusihi kila siku amuambie asili ya nguvu zao.

Siku moja Samusoni akamuambia, "Ukinifunga kwa kamba mbichi saba, halafu nitakuwa zaifu, nami nitakuwa kama mutu mwengine." Ilikuwa kweli? Sababu gani alikuwa na nguvu? (Acha wanafunzi wajibu)

Wakati Samusoni alikuwa akilala, Delila alimufunga na kamba mbichi. Alilalamika, "Samusoni, Wafilistini ni juu yako!"

Samusoni aliamka na kuvunja kamba kama uzi wa kitani. Samusoni alidanganya Delila na Wafilistini!

Shauri gani unamupa sasa Samusoni? (Musemezane murudi kwao Israeli. Omba Mungu amusamehe. Maisha yake ipendeze Mungu).

Kuliko kufanya vile, Samusoni alibaki na Delila. Siku kisha siku Delila alimwambia, "Hunipendi mimi kweli," akasema, "Umenizihaki tu!"

Mara pili Samusoni anamudanganya kuhusu siri ya nguvu zake. Kisha siku moja, hangeliweza kuendelea kuvumilia usumbufu wake. "Nyele zangu hajakatwa bado, Delila. Mimi ni munaziri. Nyele zangu zikikatwa nitakuwa bila nguvu sawa watu wengine wote!"

Bila kufikiri, Samusoni alienda kulaza kichwa chake juu ya magoti ya Delila. Alituma waite Wafilistini wafike kunyoa kichwa chake. Wakati Samusoni aliamka, alitaka kupiganisha waadui zake sawa mbele. Lakini alikuwa muzaifu kama mutoto mudogo! Uchungu gani! Aliasi Mungu hakuwa pamoja naye tena.

Onyesha taswira 15b (Ondoa kitu kilichoifunika): Wafilistini walitoboa macho ya Samusoni na akawa kipofu. Kisha walimufungia gerezani mwao pa Gaza. Pale wakamufunga sawa nyama na kumufanya mwenye kusaga.

4. Kifo cha Samusoni (Waamuzi 16:21-31)

Sawa vile majuma na miezi ilipita, nyele za Samusoni zilianza kuota. Alikuwa na muda wa kifikiri wakati alikuwa akisaga mbegu. Kwa mwisho aligeukia Bwana na kutubu juu ya njia zake za zambi. (Kazisha: hakuna kuchelewa (mwisho) kwa kutubu).

Siku moja Wafilistini walikuwa na siku kuu ya Dagoni sanamu yao. Walisema, "mungu wetu alituokoa katika mikono ya Samusoni. Tosheni Samusoni gerezani kusudi Atuchee!"

Kijana mumoja aliongoza Samusoni toka gereza hadi hekaluni. Samusoni akamuwambia, "Uniongoze niguse nguzo zinazobeba hekalu kusudi nizitegemee." Pale Samusoni aliomba, "Ee Mungu, ikikupendeza unipe nguvu za kujilipiza kisasi juu ya Wafilistini kwa ajili ya macho yangu mawili." Mungu alisikia ombi lake.

Onyesha taswira 16: Samusoni akakamata ti nguzo na nguvu zake zote. Krash! Hekalu lote likaanguka na Wafilistini 3000 walikufa pamoja na Samusoni.

Mwisho mubaya gani kwa mutu ambae kuzaliwa kwake kulitangazwa na malaika! Sababu gani maisha ya Samusoni ilikuwa na mwisho mubaya? (**Muzungumuze:** aliasi Mungu kwa uchoyo, kutokutii, kupenda kufuata njia zake, kupenda kutimiza tamaa zake pamoja na wasioamini).

Mwalimu: Somea wanafunzi wako polepole (Amosi 3:3; 1 Wakorinto 7:39 na 2 Wakorinto 6:14). Mungu anaamuru Wakristo wasioe wasioamini. Agiza wanafunzi wako wasifanye urafiki na wasioamini sababu urafiki unaongoza kwa ndoa. Onyesha kwa mukazo, kama kuwa na njia za upekee ni uasi kwa Mungu. Ile inaleta huzuni na ukosefu. Uwakumbushe shabaha ya somo. Walikombolewa na Kristo na hawaishi tena juu yao wenyewe. Wale wanaunga urafiki na wasioamini hawapendeze Mungu!

Historia ya maisha ya Samusoni si ya kupendeza. Mara kwa mara alitimiza kazi yake juu ya wafilistini. Lakini kwa sababu alichagua kujipendeza aliasi Mungu, alipata mateso mengi. Munakuwa kwa upande wa Mungu? (Kumbusha wanafunzi namna wanaweza kufahamu kama wanapendeza Mungu). Munapendeza Mungu ao munamuasi?

(Mwalimu: Tumia taswira ndani ya jalada ya mwisho kwa kukazisha kama Mungu aliendelea kusamehe taifa lake lililomuasi wakati lilitubu kwa kweli. Kazisha kama inawezekana kwa wakristo kugeuka waasi wakubwa kama wamepotoka toka maadibisho ya Mungu. Vilevile bila kutubu, wataishi maisha ya uchungu. Na wakiendelea vile mbele ya Mungu, wataendelea katika uchungu wa milele bila malipo. Angalia 1 Wakorinto 3:10-15; 2 Wakorinto 5:10).